**Annexure A: MAJUKUMU YA KAZI**

**Cheo:** Housekeeping Staff / Domestic Worker

**Kiongozi wako:** Housekeeping Manager

**Maelezo ya hiki cheo:**

Ni jukumu la Housekeeping staff kuhakikisha anafanya usafi vizuri maeneo yote ya hospitali, kwa kufuata taratibu na miongozo ya ufanyaji usafi. Kwa lengo la kutoa huduma nzuri na inayokidhi viwango vya usafi na matarajio ya wagonjwa.

**Jukumu moja moja:**

- Futa vumbi kwa kitambaa kinyevunyevu kwenye meza, viti, makabati, vioo, milango, madirisha n.k.
- Deki sakafu za vyumbani, koridoni, ngazi, vyooni, mabafuni n.k.
- Hakikisha unachanganya kiasi cha dawa/ vimiminika vya kufanyia usafi vizuri kama inavyotakiwa kwenye kanuni za usalama makazini.
- Hakikisha kila choo kina sabuni ya maji, toilet paper na tissue za kukaushia mikono
- Hakikisha saa za ukutani zinaonyesha majira ya sahihih, taa na AC zinawaka vizuri.
- Toa nguo na mashuka machafu wodini na vipeleke eneo la kuhifadhi nguo chafu tayari kwa kwenda kufuliwa.
- Toa uchafu kwenye ndoo za taka za vyumbani na koridoni na peleka moja kwa moja sehemu sahihi.
- Weka mifuko misafi kwenye ndoo za taa.
- Zingatia rangi za mifuko unapotoa taka na kwenda kuziweka sehemu husika, usichanganye rangi (Nyekundu, Njano na Nyeusi).
- Weka magauni, mashuka na mataulo safi wodini kila asubui.
- Pokea malalamiko ya wagonjwa yanayohusiana na Housekeeping na yawasilishe kwa uongozi.
- Andaa na hifadhi vifaa/ vitendea kazi vya usafi vizuri.
- Mjulishe kiongozi wako iwapo kuna kifaa cha usafi kinakaribia kuisha au kimeharibika.
- Mjulishe kiongozi wako haraka kama kuna uharibifu au upotevu wowote eneo lako la kazi.
- Hakikisha eneo la kutunza vifaa vya usafi ni safi na liko kwenye mpangilio mzuri muda wote.
- Hakikisha umeweka kumbukumbu vizuri ya nguo zilizochukuliwa kwenda kufuliwa.
- Hakikisha unakagua nguo zilizotoka kufuliwa kama ziko idadi sahihi, zimepigwa pasi na kwenye hali ya usafi kama inavyotakiwa.
- Kusogeza au kuhamisha vifaa vya ofisini au wodini kama utakavyoelekezwa na kiongozi uongozi.
- Kazi zingine za ziada kama utakavyoelekezwa na uongozi.

**Ya kuzingatia:**
Kuwahi kuingia kazini kama ulivyopangwa kwenye shifti
Kuwepo kwenye eneo ulilopangiwa kazi muda wote
Kuvaa sare ya kazi muda wote
Kutoa taarifa mapema endapo utachelewa au hutofika kazini.